**TAARIFA YA MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI KWA VYOMBO VYA HABARI TAREHE 05 JANUARI, 2026**

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana!***

**“Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”**

***Ndugu wanahabari,*** Awali ya yote, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa siku ya leo, tukiwa na afya njema.

***Ndugu wanahabari,*** kipekee, napenda nitumie nafasi hii kumshukuru **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuipatia Wizara ya Madini miongozo thabiti inayolenga kuikuza Sekta ya Madini kwa kuongeza fursa za ajira kwa vijana ili waweze kuzalisha zaidi na hatimaye kuifanya Sekta hii kuwa na mchango katika Pato la Taifa.

***Ndugu wanahabari,*** napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini, Mhe. Dkt. Stephen Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri; Eng. Yahya Samamba, Katibu Mkuu; Ndugu Msafiri Mbibo, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Viongozi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika

kutekeleza majukumu yangu na kutekeleza majukumu yao kwa kujituma, kwa tija na ufanisi mkubwa. Kwa pamoja tunakiri kuwa na dhamira moja tu ambayo ni kuhakikisha tunatekeleza na kufikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya Watanzania na Taifa letu kwa ujumla.

***Ndugu wanahabari,*** Serikali kupitia Wizara ya Madini imeendelea kuhakikisha rasilimali madini inakuwa na manufaa kwa Watanzania wote kupitia makusanyo ya moja kwa moja yatokanayo na shughuli mbalimbali za madini; kuhakikisha uwepo wa fursa za ajira kwa Watanzania kupitia taaluma na ujuzi walio nao pamoja na utoaji wa huduma katika miradi ya madini; na ununuzi katika migodi unafanyika kwa kutoa kipaumbele kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

***Ndugu wanahabari,*** kutokana na jitihada hizo, mapato ya Serikali yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 526.722 sawa na asilimia 111 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia kiasi cha Shilingi trilioni 1.071 sawa na asilimia 107.13 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2024/2025. Aidha, kwa mwaka 2025/2026 Wizara imewekewa lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi trilioni 1.2 ambapo katika kipindi cha miezi sita (6), kuanzia Julai, 2025 hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2025, jumla ya kiasi cha Shilingi bilioni 653.139 kimekusanywa sawa na asilimia 108.86 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 600 kwa kipindi husika na sawa na asilimia 54.42 ya lengo la mwaka. **Jedwali 1** linaonesha mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025.


**Jedwali 1: Makusanyo ya maduhuli kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025**

| Mwaka | Lengo la Makusanyo | Makusanyo Halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 526,722,547,000.00 | 584,822,732,651.00 | 111 |
| 2021/2022 | 650,000,000,000.00 | 624,614,761,900.65 | 96 |
| 2022/2023 | 822,018,203,000.00 | 677,734,778,784.74 | 82 |
| 2023/2024 | 882,121,205,000.00 | 754,697,906,468.11 | 85 |
| 2024/2025 | 1,000,000,000,000.00 | 1,071,273,845,900.88 | 107.13 |

***Ndugu wanahabari,*** katika miradi ya madini tumeshuhudia ongezeko la ajira kwa Watanzania kutoka ajira 6,668 kati ya ajira 7,003 sawa na asilimia 95 kwa mwaka 2018 hadi kufikia ajira 18,853 kati ya ajira 19,356 sawa na asilimia 97 kufikia Desemba 2024.

Aidha, katika nafasi zinazohitaji kupata uzoefu kutokana na kukua kwa teknolojia duniani, kumekuwa na utaratibu wa Kisheria wa urithishwaji wa Watanzania kwa nafasi zinazoshikiliwa na Wataalamu wa Kigeni. Hii ni kutimiza azma ya Serikali ya kuongeza idadi ya Watanzania wanaoshikilia nafasi za uongozi katika Kampuni za uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini.


***Ndugu wanahabari,*** Mfano mzuri ni mgodi wa dhahabu wa North Mara unaomilikiwa na Kampuni ya Twiga Minerals Corporation (Barrick Gold) ambapo nafasi zote za juu za uongozi zinashikiliwa na Watanzania. **Kielelezo 1** kinaonesha ulinganisho wa ajira za watanzania na wageni mwenendo wa ongezeko kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2024.




**Kielelezo 1: Hali ya Ajira Migodini**

***Ndugu wanahabari,*** katika manunuzi ya bidhaa na utoaji huduma migodini, Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kuweka usimamizi thabiti kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwa Watanzania kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura ya 123. Usimamizi huo umekuwa na matokeo chanya kwa kuongeza idadi ya Watanzania wanaotoa huduma na kuuza bidhaa kwa wamiliki wa leseni za madini nchini.

Manunuzi ya huduma na bidhaa kwa Kampuni za Kitanzania yameongezeka kutoka kiasi cha Shilingi trilioni 1.85 kati ya manunuzi ya huduma na bidhaa za jumla ya kiasi cha Shilingi trilioni 3.01 sawa na asilimia 62 kwa mwaka 2018 hadi kufikia Shilingi trilioni 4.41 ambayo ni sawa na asilimia 88 ya kiasi cha Shilingi trilioni 5.00 ya manunuzi yote yaliyofanyika mwaka 2024. **Kielelezo 2** kinaonesha manunuzi ya bidhaa na huduma kwa wamiliki wa leseni za madini.




**Kielelezo 2: Manunuzi ya bidhaa na huduma kwa wamiliki wa leseni za madini**

***Ndugu wanahabari,*** katika kuhakikisha Watanzania wananufaika na fursa ya ajira migodini, Wizara kupitia Tume ya Madini imekuwa ikihamasisha ujenzi wa viwanda vya bidhaa zinazohitajika kwa wingi katika migodi yetu. Kupitia uhamasishaji huo, Kampuni mbalimbali zimeanza kujitokeza kuwekeza katika kutengeneza baadhi ya bidhaa zinazohitajika migodini. Kampuni hizo ni pamoja na Rock Solutions Limited, Max Steel na East Africa Conveyors Supplies Limited. Viwanda hivi vimejengwa kwa kushirikiana na kampuni zinazozalisha bidhaa hizo na kusambazwa katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania.

***Ndugu Wanahabari,*** katika kufanikisha lengo la Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini kwa kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi. Tume ya Madini imeanzisha utaratibu wa kuendesha Majukwaa ya Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania

katika Sekta ya Madini kila mwaka ambayo yanahusisha Wamiliki wa leseni, watoa huduma na wasambazaji bidhaa migodini, Taasisi mbalimbali za Serikali, Wizara ya Madini na Taasisi zake. Lengo la majukwaa hayo ni kutathmini utekelezaji wa kanuni za ushirikishwaji wa watanzania, kujadili changamoto zinazojitokeza na kuweka maazimio ya nini cha kufanya ili kuboresha. Hadi sasa Tume ya Madini imeshaendesha majukwaa manne ya ushirikishwaji wa watanzania kwa mafanikio makubwa.

Aidha, Majukwaa haya huambatana na Maonesho ya Bidhaa na huduma kutoka kwa Kampuni za Uchimbaji wa Madini na kampuni za utoaji huduma na Bidhaa migodini ili kuonesha aina na ubora wa huduma na bidhaa zinazohitajika kwa wamiliki wa migodi nchini ili Watanzania wengi waweza kushiriki na kuchangamkia fursa hizo kwa manufaa mapana ya Taifa.

***Ndugu Wanahabari,*** Serikali kupitia Wizara ya Madini imefanya marekebisho ya Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania za mwaka 2018 ambapo Tume ya Madini mara kwa mara itatangaza kupitia Kanuni ya 13A orodha ya bidhaa na huduma ambazo zinatakiwa kutolewa na kampuni za Kitanzania ambazo zinamilikiwa kwa asilimia 100 na Watanzania, lengo likiwa ni kuongeza wigo wa ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Madini kwa manufaa mapana ya taifa.

Kwa awamu ya kwanza tarehe 14 Novemba, 2025 Tume ya Madini ilitangaza orodha ya bidhaa na huduma zinazotakiwa kutolewa na kampuni zinazomilikiwa na kampuni za kitanzania kwa asilimia 100. Vitu

vilivyoainishwa kwenye orodha hiyo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali 2**.

**Jedwali 2: Huduma zinazopaswa kutolewa na Watanzania kwa Asilimia 100**

| Na. | Aina ya Huduma |
|---|---|
| 1. | *Supply of General Lubricants* |
| 2. | *Supply of Chain Link Fencing, Wire Netting, Barbed Wire* |
| 3. | *Supply of Cement and Building materials* |
| 4. | *Supply of Metal/PVC Core Trays* |
| 5. | *Supply of Overalls and Work Clothes and PPEs* |
| 6. | *Haulage, Logistics and Transportation Services* |
| 7. | *Warehousing, Clearing and Forwarding* |
| 8. | *Catering Services, Camp Management, Cleaning and Laundry* |
| 9. | *Legal Services* |
| 10. | *Supply of Activated Carbon* |
| 11. | *Supply of Cable Bolt and Accessories, Split Set, Rebars, Mining Mesh -Underground Support Materials* |
| 12. | *Supply of Explosives and Accessories* |
| 13. | *Owner Mining Prohibited in favour of Contract Mining – Surface operations (Open Cast mining services including Contract mining, Drilling, Blasting, Haulage)* |
| 14. | *Vehicle Hire* |
| 15. | *Power Rental and Captive power supply* |
| 16. | *Crushing, Civil, Building and Construction of access/haul roads & other infrastructure, etc.* |

| Na. | Aina ya Huduma |
|---|---|
| 17. | *Geophysical Ground-based Survey; Mapping, Pitting and Trenching* |
| 18. | *Land Valuation and Resettlement* |
| 19. | *Supply of Linning Material (Liners)* |
| 20. | *Supply of Chemicals and Reagents* |

***Ndugu Wanahabari***, nitumie nafasi hii kutoa rai kwa Watanzania, kuendelea kuhakikisha wanapata utaalamu sahihi unaohitajika katika shughuli za madini ili kuweza kuwa miongoni mwa wanaostahili kupatiwa fursa za ajira katika migodi sambamba na fursa za utoaji huduma katika miradi hiyo. Aidha, watoa huduma wote wahakikishe wanatoa huduma bora kulingana na viwango stahiki ili kuendelea kuaminika katika utoaji wa huduma husika.

***Ndugu wanahabari,*** kwa kumalizia, niwasisitize wawekezaji wote kuzingatia Sheria ya Madini Sura 123 na utekelezaji wa Kanuni za *Local Content* sambamba na kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo katika miradi ya madini ili kukabiliana na changamoto ya ajira kwa manufaa ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Wizara ya Madini inaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi wenye nia ya kufanya uwekezaji wenye tija na kukuza uchumi wa taifa letu kutokana na uvunaji wa rasilimali madini.

**“ASANTENI SANA”**